**WARAKA KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, Mh. JOHN POMBE MAGUFULI, KUHUSU HALI YA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA TANGU KUMALIZIKA KWA MUDA WA MAKAMISHNA WA TUME JANUARI 2018**

**Msingi wa Kisheria wa Tume**

**Mh. Rais,** kuhusu kichwa cha waraka huu hapo juu, Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania wanapenda kukukumbusha juu ya hali ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG). Tume ya Haki za Binadamu ni chombo muhimu ambacho kilichoanzishwa chini ya Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, 2001. Pia ni chombo cha kikatiba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 hususani ibara ya 129 (1).

**Mh. Rais,** Kikatiba na kisheria Tume imepewa mamlaka ya aina mbili, yaani; kutumikia umma na kuwa kama mshauri mkuu wa serikali na mihimili mingine pale ambapo masuala ya haki za binadamu yanahusika nchini. Majukumu ya Tume pia yametolewa kwenye ibara ya 130 ya Katiba. Majukumu haya yanajumuisha; kuhamasisha ulinzi wa haki za binadamu, kukuza, kuimarisha kuheshimu haki za binadamu kwa mujibu wa sheria za nchi, kupokea malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu, kufanya uchunguzi juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu na kutoa mapendekezo, Pia tume hutoa na kueneza ufahamu juu ya masuala ya haki za binadamu pamoja na kuishauri serikali na taasisi zingine zinazohusika na masuala ya haki za binadamu na utawala bora nchini.

**Muundo wa Tume**

**Mh. Rais,** tunaomba kukujulisha kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, 2001, uwepo wa Tume unajumuisha muundo ufuatao;

a) **Mwenyekiti wa Tume**
b) **Makamu Mwenyekiti, (ambaye atateuliwa kwa kuzingatia kanuni kwamba endapo Mwenyekiti ni mtu anayetoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, yeye atakuwa ni mtu wa kutoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano)**
c) **Makamishna wengine wasiozidi watano**
d) **Makamishna Wasaidizi**
e) **Katibu Mtendaji wa Tume**

Ni muhimu kutambua kwamba, Tume inaongozwa na Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais. Tume pia ina Makamishna na Makamishna Wasaidizi ambao pia wanateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Kamati ya Uchaguzi. Hawa ndio viongozi wa juu wa Tume ambao kuwepo kwao kunasababisha Tume kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**Kutokuwepo kwa Tume**

**Mh. Rais,** hata hivyo, inahuzunisha kwamba tangu Januari 2018 ambapo muda wa uongozi wa Mwenyekiti, Makamishna na Makamishna Wasaidizi umeshaisha, viongozi hawa muhimu katika Tume bado hawajateuliwa licha ya kuwa baadhi ya wagombea waliovutiwa waliomba nafasi hizo na walifanyiwa mahojiano. Cha kushangaza, Makamishna hao wa zamani walikuwa na uwezo wa kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu lakini hakuna hata mmoja aliyeteuliwa tena tofauti na awamu zilizopita ambapo Makamishna walitumikia kwa miaka sita baada ya kuteuliwa upya na Rais.

Kikanuni, Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 Tume inasemekana kuwa kamili au kuwepo kisheria wakati mwenyekiti wake na makamishna wapo kwenye ofisi. Zaidi ya hapo, Katibu Mtendaji wa Tume pia amestaafu karibu mwezi mmoja sasa na nafasi yake bado iko wazi. **Mh. Rais,** kwa mujibu wa uchambuzi huu wa kisheria ambao umefanywa na THRDC, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haipo kwa karibu mwaka sasa.

**Madhara kwa Taifa**

**Mh. Rais,** Raia wa Tanzania wamekuwa wakihoji kwa nini Tume haina uongozi kwa karibu mwaka sasa? Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania kama shirika mwanvuli la watetezi wa haki za binadamu nchini Tanzania ambalo linawakilisha wanachama wake zaidi ya 150 linafatilia kutokuwepo kwa Tume kwa karibu mwaka sasa ambapo masuala ya ukiukwaji wa haki za binadamu nchini yanashindwa kukemewa.

- THRDC inaamini kwamba masuala mengi ya haki za binadamu hayachukuliwi hatua kwa sababu Tume haipo kisheria.
- THRDC na wadau wengine wa haki za binadamu sasa hawana nafasi ya kushirikiana na tume katika maeneo mengi ya haki za binadamu.
- Sekretarieti ya Tume haiwezi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi
- Tume imeshindwa kuhudhuria mikutano mbalimbali ya kikanda na ya kimataifa ya haki za binadamu
- Tume imeendelea kupata mgawanyo hafifu wa rasilimali
- Tume imeshindwa kuishauri serikali na mihimili mingine ya umma juu ya masuala ya utawala na haki za binadamu ambayo yanaathiri nchi kwa sasa
- Tume imeshindwa kupitisha mpango wake mpya wa kimkakati kwa sababu viongozi wenye mamlaka ya mwisho hawapo ofisini
- Tume imeshindwa kutoa ripoti za haki za binadamu kwa miaka mitatu iliyopita na kwa sababu ya vikwazo vya bajeti.

- Tume imeshindwa kushirikiana na serikali na wadau wengine juu ya masuala ya sera na utafiti kwa sababu viongozi hawapo ofisini.
- Tume imeshindwa kufikia viwango vya kimataifa vya Tume ya Haki za Binadamu.

**Ushiriki wa Tume katika Mikutano ya Kimataifa**

**Mh. Rais,** Kwa miaka mitatu iliyopita, ushiriki wa Tume katika mikutano ya kikanda na kimataifa haukuwa mzuri. Labda na kwa hakika ni kwa sababu ya vikwazo vya bajeti au ukosefu wa uongozi wa kupitisha baadhi ya shughuli na safari za sekretarieti ya Tume. Mnamo tarehe 22 hadi 26 Oktoba 2018, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilifanya Mkutano wake wa 63 wa kawaida. Vikao kama hivi ni muhimu sana na Tume ilipaswa kuwa imehudhuria. Hata hivyo, hakuna muwakilishi kutoka kwenye Tume aliyehudhuria mkutano huo. Kushindwa kwa Tume kushiriki katika mikutano ya kikanda na ya kimataifa ni pengo kubwa. Tume inakosa fursa ya kujifunza na kubadilishana uzoefu juu ya masuala ya haki za binadamu na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Hali ya Kifedha na Bajeti ya Tume**

THRDC pia ina mashaka na kiasi cha bajeti ambayo imekuwa ikitengwa kwa ajili ya Tume. Bajeti inayoidhinishwa na kiasi kinachotolewa kila mwaka huwa na utofauti mkubwa na husababisha mashaka makubwa kwa utekelezaji wa kazi za tume. Kwa mfano;

- Katika bajeti ya 2013/2014 kiasi kilichoidhinishwa kilikuwa TZS 3,795,802,000 na kiasi kilichopelekwa ni TZS 1, 549, 114, 131.
- Katika bajeti iliyopitishwa mwaka 2014/2015 kilikuwa TZS 4, 556, 012, 000 na kiasi kilichopelekwa ilikuwa TZS 1, 882, 505, 315.
- Katika bajeti iliyoidhinishwa ya 2016/2017 kiilikuwa ni TZS 1, 178, 854, 026 ambacho ni kidogo sana ikilinganishwa na miaka iliyopita

na kiasi kilichopelekwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2016 kilikuwa 556, 391, 226.

Majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hayahitaji uongozi tu bali pia fedha za kutosha kulingana na kanuni za Paris(Paris Principles) kuhusu Uhuru wa Taasisi za Haki za Binadamu. Kwa hiyo ni muhimu kwa serikali kutoa bajeti ya kutosha kwa Tume ili kuwezesha kutekeleza kazi zake kwa ufanisi na kwa kujitegemea. Kwa ufupi fedha hizi zinazotolewa huishia kwenye mishahara na kuendesha ofisi zote nne za Tume.

Mheshimiwa Rais, Kanuni za Paris zinazohusiana na Hali ya Taasisi za Umma zinazojulikana kama *Kanuni za Paris, 1993* zinahitaji pamoja na mambo mengine zinahitaji kuwa kila nchi inapaswa kuwa na taasisi za kitaifa ambazo zitapewa uwezo wa kukuza na kulinda haki za binadamu (Rejea Kanuni ya 1). Kwa mujibu wa Kanuni ya 2 ya Kanuni za Paris, taasisi zilizoanzishwa zitakuwa na miundombinu yao ya kutosha na bajeti ya kutosha ili kuwawezesha watumishi wake kufanya shughuli zao kwa ufanisi na bila upendeleo. Kwa hiyo ni wajibu wa kila serikali kuhakikisha taasisi za kitaifa kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora zinakamilika kiuongozi na zina fedha za kutosha kwa shughuli zao za kila siku.

**Wito Wetu**

**Mheshimiwa Rais,** ili kuepusha kushuka kwa hadhi ya Tume na Taifa letu kwa ujumla, kwa heshima na taadhima tunakuomba uangalie kwa haraka hali ya sasa ya tume. Kama Msimamizi Mkuu wa Haki za Binadamu wa kitaifa, tunakuomba uhakikishe utekelezaji wa yafuatayo:

- Kwa unyenyekevu tunakukumbusha kuwa kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mtetezi mkuu wa haki za binadamu nchini kuteua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora ili kuipa tume nguvu na uhalali wa kufanya kazi kwa ufanisi.

- Tunakuomba Mh. Rais uwateuwe Makamishna wa Tume ili Tume iwepo kisheria,
- Tunakusihi Mh. Rais umteue Katibu Mtendaji wa Tume
- Kwa Jitihada ambazo Mh. Rais wetu amezionesha katika teuzi mbalimbali za viongozi wa serikali na mashirika ya umma, tunaomba aendelee nazo pia katika kuteua Makamishna wa Tume ambao ni sehemu ya mipango yake mizuri katika kuleta maendeleo.
- Tunatoa wito kwa serikali ya Tanzania na Bunge kuboresha kiwango cha fedha zinazotengwa kwaajili ya shughuli za Tume kila mwaka.

**Imetolewa leo, tarehe 28 Novemba 2018**

**Na:**

**Mratibu wa Kitaifa**

**Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC**

**Onesmo Olengurumwa**

**Nakala kwa:**

**Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

**Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Waziri wa Katiba na Sheria**

**Spika wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania**